

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

610


UALIMU

Muda: Saa 3

Year: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** katika kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vyote vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



2

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Umepewa jukumu la kukusanya taarifa za wanafunzi wa Darasa la Pili katika shule yako. Ni mambo gani utakayozingatia wakati wa kutekeleza jukumu hilo? Orodhesha mambo manne.
2. (a) Eleza kwa kifupi maana ya uhawilisho hasi wa maarifa.
(b) Fafanua kwa kifupi mambo matatu yanayosababisha uhawilisho hasi.
3. Mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja kimoja yana faida na hasara. Kubaliana na kauli hii kwa kutoa faida mbili na hasara mbili.
4. Katika hotuba yake ya kwanza baada ya kuteuliwa, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia alisisitiza umuhimu wa nchi kuwa na mtaala wa aina moja. Je, faida zipi zitapatikana endapo msisitizo huo utatekelezwa? Toa hoja nne.
5. Matokeo ya wanafunzi saba yalikuwa kama ifuatavyo: 27, 65, 56, 53, 72, 63 na 56. Tafuta:
(a) Wasitani (b) Modi
(c) Mediani (d) Mfiko
6. Kwa kutumia hoja nne, weka bayana sifa za suala zuri la utafiti.
7. Mwalimu mkuu wa shule ya msingi Manumbu aliagiza kila mwalimu kufanya tathmini ya somo lake analofundisha. Ni hatua zipi walimu hao wanapaswa kuzifuata wakati wa uandishi wa matokeo ya tathmini hizo? Toa hoja nne.
8. Umepewa jukumu la kubainisha mifumo mbalimbali ya elimu katika nchi yako. Ni sifa zipi utazitumia kubainisha mfumo rasmi wa elimu? Eleza sifa nne kwa kifupi.
9. Kwa kutumia hoja nne, eleza kwa kifupi madhumuni ya elimu ya watu wazima kama yalivyoelezwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1970.
10. Katika mahafali ya kuhitimu Elimu ya Msingi katika Shule moja ya Msingi, Afisa Elimu wa Mkoa aliipongeza shule hiyo kwa kuwa na uongozi bora. Ni viashiria gani alivitumia kubaini ubora wa uongozi wa shule hiyo? Toa hoja nne.

SEHEMU B (Alama 60)
Jibu maswali yote katika sehemu hii.

11. Ukuaji wa mtoto baada ya kuzaliwa huweza kuathiriwa na mambo mbalimbali. Eleza mambo sita.
12. Chambua kwa kina faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya kazi mradi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
13. Umepewa jukumu la kutunga maswali ya "Kweli au Si kweli." Eleza mambo sita unayopaswa kuyazingatia katika kutekeleza jukumu hilo?
14. Kwa kutumia mifano halisi, fafanua wadau sita wa elimu ya watu wazima waliotoa mchango wao katika kuendeleza elimu hiyo hapa Tanzania.